# TAARIFA HALISI NAMBA NANE

## WATOTO NA VIJANA: CHANZO CHA HOFU, "DIRISHA LA MATUMAINI"

Duniani kote, vijana wanne wa umri wa kati ya miaka 15 na 24 huambukizwa VVU kila dakika - yaani kiasi cha vijana 6,000 kwa siku. Takriban theluthi mbili ya vijana wenye VVU wanaishi Afrika, kusini mwa Jangwa la Sahara.

Katika Afrika, kusini mwa Jangwa la Sahara nusu ya maambukizi mapya yote hivi sasa hutokea miongoni mwa umri wa miaka 15 hadi 24. Wasichana na wanawake wanaathirika sana, ambao ni theluthi mbili ya walioambukizwa kati ya umri wa miaka ya 15 hadi 24. Kwa ujumla, takriban mara mbili ya wanawake wenye umri huo wanaambukizwa kuliko wanaume; katika baadhi ya nchi kama vile Afrika Kusini, uwiano unafikia tano kwa moja.

Takwimu hizi za kusikitisha zinadhihirisha kuwa, haja ya kufanya uzuiaji wa maambukizi ya VVU inahitaji kupewa vyama vya hiari kuwa kipaumbele. Kupunguza idadi hii kunahitaji juhudi za dhati za kuwafikia vijana wadogo ambao bado hawajajihusisha zaidi na ngono, na ambao wanawakilisha **"dirisha la matumaini" ili kupunguza maambukizi.**

Viwango vya juu vya maambukizo vilivyopo vinaashiria ukosefu wa jumla wa taarifa kuhusu VVU/UKIMWI miongoni mwa vijana:

- Utafiti unaonyesha kuwa ni takriban nusu tu ya vijana wote katika kanda ya Afrika wana taarifa za kutosha kuhusu VVU.

- Chini ya theluthi moja ya wanawake vijana wenye umri wa kati ya miaka 15-24 wanaelewa namna ya kujiepusha na maambukizi. Vijana wa kiume wanaelewa zaidi kwa asilimia 20.

### Vijana hasa wasichana, wana haki ya:

- Kupata taarifa za kuaminika kuhusu uzuiaji wa VVU.
- Kushiriki katika utayarishaji na usambazaji wa ujumbe mbalimbali kuhusu VVU/UKIMWI.
- Kupata huduma rafiki na nyeti ya kupima VVU, tiba ya magonjwa ya ngono na kondomu.
- Kulindwa dhidi ya ubakaji, unyanyasaji, utumiaji nguvu na ulazimishaji katika kufanya tendo la ngono.
- Hata katika nchi zenye ueneaji mkubwa wa maradhi (kama vile Cameruni, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Equatorial Guinea na Sierra Leone), chini ya asilimia 20 ya wanawake vijana wenye umri wa miaka 15-24 wana taarifa ya kutosha kuhusu uzuiaji wa VVU.
- Asilimia 20 ya wanafunzi wa Sekondari nchini Botswana, ambayo ni miongoni mwa nchi zenye kiwango cha juu cha ueneaji wa VVU, wasichana wanaweza kueleza kwa kumwangalia tu, iwapo mwenza ana VVU au hapana.
- Nchini Nigeria, asilimia 60 ya watu wako chini ya umri wa miaka 24, na hivyo kuwa hatarini zaidi

kuambukizwa VVU; ambayo ni nchi ya tatu yenye idadi kubwa ya watu wanaoishi na VVU/UKIMWI duniani (kiasi cha watu milioni 3.6, mwaka 2003).

## Hatari maalumu, Mahitaji maalum

Katika nchi za Afrika, kusini mwa Jangwa la Sahara, vijana walio hatarini zaidi kutoelewa kuhusu VVU ni:

- Watoto wa mitaani.
- Yatima.
- Wasichana vijana walio katika umri wa balehe.
- Wakimbizi.
- Watumiaji dawa za kulevya.
- Askari Watoto.
- Wasichana na Wavulana wanaojihusisha na biashara ya ngono/ukahaba.

Matatizo makubwa zaidi wanayokabili vijana yanahitaji ufumbuzi kabambe. Ili kuwalinda, mambo yafuatayo yanatakiwa kufanyika;

- Taarifa za kuaminika, zinazoeleweka kuhusu maambukizi na uzuiaji, zikiwemo juhudi maalumu za kuwahusisha vijana na kuwaelimisha hasa wasichana waliovunja ungo kuhusu ngono na hatari ya VVU.

- Huduma rafiki za afya kwa vijana pale ambapo wako tayari kupima maambukizo ya magonjwa ya ngono na VVU, watoa huduma wapatiwe mafunzo ya kuwahudumia vijana kwa njia ya kirafiki.

- Mabadiliko ya sheria na mitazamo ya kijamii na kupiga vita unyanyapaa, ubaguzi na ulazimishaji na kutumia nguvu katika ngono. Mabadiliko ya sheria zinazokataza kupima bila ya ridhaa ya wazazi.

- Upatikanaji wa kondomu

- Ushiriki wa vijana walio katika umri wa balehe katika kubuni ujumbe wa kubadili tabia/uzuiaji na kuwasilisha kwa makundi rika.

Elimu ya Stadi za Maisha ni shughuli ya kuzuia maambukizi ya VVU inayofanyika katika nchi nyingi ili kuwasaidia vijana kutekeleza haki yao ya kulindwa dhidi ya VVU. Hasa wasichana, wanajua kwamba wanayo haki ya kudai wenzi wao watumie kondomu, kukataa ngono, na uhuru wa kujieleza kuhusu masuala ya ngono. Kuzidisha Elimu ya Stadi za Maisha kutasaidia kuharakisha uzuiaji wa VVU barani Afrika.

## Dirisha la matumaini

Watoto ambao hawajihusishi na ngono pia wanahitaji taarifa kuhusu uzuiaji wa VVU na kuwapa taarifa hiyo kutasaidia kupunguza kasi ya kuenea kwa Virusi Vya UKIMWI katika kizazi hicho.

Tofauti na suala gumu zaidi la kuwasaidia vijana walio katika umri wa balehe wanaojihusisha na ngono kubadili

tabia/mienendo na mitazamo waliyojifunza, kwa watoto wadogo kazi ni rahisi zaidi: **kujenga tabia/mienendo na mitazamo kuanzia umri mdogo, ikiwa pamoja na:**

- kuwazuia kuanza tendo la ngono mapema.
- Kuelewa athari za kuwa na wenzi wengi kila ngono/wapenzi wengi.
- Kutumia Kondomu wakati wa kufanya tendo la ngono.
- Kuwaheshimu na kuwaonea huruma watu wanaoishi na VVU/UKIMWI.

Mtaala wa masomo ya shule una nafasi kubwa katika kufundisha vijana kuhusu uzuiaji, lakini si shule nyingi zimeingiza elimu ya VVU/UKIMWI katika mtaala wao.

Ili kupunguza kasi ya maambukizo ya VVU miongoni mwa vijana na watoto, kunahitajika juhudi za jamii yote za kueneza taarifa na stadi za maisha, na kupunguza tabia za ngono hatarishi:

- Nchi hazina budi kuwekeza haraka katika utayarishaji na utekelezaji wa mtaala unaolingana na umri kuhusu VVU/UKIMWI.

- Walimu hawana budi kufundishwa namna ya kushughulikia masuala haya kwa uhakika na bila kuaibisha.

- Wazazi na viongozi wa dini na jamii hawana budi kutilia mkazo ujumbe wanaopata watoto shuleni. Kunahitajika kuwapo na mazungumzo ya wazi katika mazingira tofauti – nyumbani, katika vituo vya maendeleo ya jamii, katika matukio ya utamaduni, jamii na dini.

- Viongozi wa Kitaifa hawana budi kujenga mazingira ya kusaidia kwa ajili ya uzuiaji kwa kutoa huduma zinazotakiwa na kusisitiza matumizi ya sheria zinazowalinda watoto na maambukizo ya VVU na wafanyaji ngono.

- Sauti ya vijana haina budi kuheshimiwa na kusikilizwa.

- Vyombo vya habari havina budi kutayarisha programu za ubunifu kwa watoto na vijana walio katika balehe ili kusisitizia ujumbe wa uzuiaji, kufanya juhudi maalumu ya kuwafikia vijana walio hatarini zaidi kuambukizwa.